



COUNTY ASSEMBLY OF MOMBASA
THE HANSARD

Wednesday, 31st July, 2024

Third Assembly – Third Session
FIFTY EIGHTH SITTING

*[The County Assembly met at 10:15a.m at the County Assembly Buildings]
[The Deputy Speaker (Honourable Fadhili Mwalimu Makarani) in the Chair]*

PRAYERS

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Have your seats Members. Clerk, please confirm if there is a quorum?

[Lack of quorum]

Serjeant-At-Arms, please ring the quorum bell.

[Serjeant-At-Arms rung the quorum Bell]

Yes Clerk, please confirm if there is quorum we proceed?

[Clerk confirmed quorum]

Yes, Clerk Order number one please?

COMMUNICATION FROM THE CHAIR
STUDY VISIT BY MOMBASA JITAMBUE INITIATIVE

Good afternoon Honourable Members. I wish to bring to the attention of this Honourable House that we have visitors from Mombasa, Jitambue Initiative. I recognize the presence of the Members which consists of..., if you hear your name please stand up and bow:

1. Ms. Zahida Mohamed Slim
2. Ms. Fatima Hassan
3. Ms. Rumana Mohamed
4. Ms. Muna Ismail
5. Mr. Abdulrahman Shariff Omar
6. Mr. Steve Onyona

7. Mr. Mohamed Salim
8. Ms. Filsaan Dahir
9. Ms. Jamila Zubeir Osman
10. Ms. Mariam Hussein
11. Ms. Suaad Abdunnassir
12. Ms. Khalila Fuad
13. Ms. Yusra Ishak
14. Ms. Twalha AbdulKadir
15. Ms. Ahlam Mohamed
16. Ms. Zeinab Maganga

On behalf of the Assembly, I welcome you all to the County Assembly of Mombasa *karibuni sana* and will let two Honourable Members to give a welcoming remark to the guests; Honourable Abdirahman and Honourable Florence please, Honourable Abdulrahman please.

Hon. Abdirahman Abdikadir: Thank you Mr. Speaker for giving me the opportunity to usher in our guests today. Mine is to welcome them to these noble chambers where we transact business that is crucial to the residents of Mombasa. This is the House where laws are passed, this is the House that oversees the Executive and as leaders we are very happy to host them here today and make sure that they at least take one or two things back to the electorates; with those few remarks Mr. Speaker thank you very much for the opportunity *karibuni sana mujihisi muko nyumbani*. Thank you.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Florence Kachumbo?

Hon. Kachumbo: Thank you Mr. Speaker for this opportunity. I would like to thank God for the gift of life. I would like to welcome the Jitambue Initiative for joining us in our daily work, here we represent the people in *mashinani* to meet their needs and I would like to encourage each one of you as you watch us here, I am sure you would have something to go and tell the people on how the Members of the County Assembly are doing to represent you people. Thank you.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes Clerk?

MOTION

MEASURES TO ADDRESS SUBSTANCE ABUSE AND MENTAL HEALTH AMONG THE YOUTH IN
MOMBASA COUNTY

Yes, Honourable Frankline Makanga please read your Motion.

Hon. Makanga: Thank you Mr. Speaker. Mr. Speaker I beg to move the following Motion;

AWARE that the Mombasa County Alcoholic Drinks Control Act, 2014 regulates the production, sale and consumption of alcoholic drinks within the County;

FURTHER AWARE THAT the National Drugs and Psychotropic Substances Control Act, Revised Edition (2012) 1994 and the Mental Health Act, Revised Edition, 2012 (1991) provide a legal framework for regulating illegal drugs and supporting mental health;

Observing that substance abuse among the youths in Mombasa County has reached alarming levels, contributing to increased crime rates, school dropouts and health complications;

Highlighting that mental health issues, exacerbated by substance abuse, have led to increased rates of depression, anxiety and suicide among the youth;

Noting with concern that the Healthcare Systems Task Force in the County formed by HIS Excellence the Governor, acknowledged the need to establish rehabilitation centers by repurposing Mrima and Marimani healthcare facilities to address drug and substance abuse issues;

Alarmed that despite the recommendations of the Healthcare Systems Task Force, the proposal to repurpose Marimani and Mrima hospitals into rehabilitation centers has not yet been implemented;

Disturbed that the County does not have well-equipped rehabilitation centers specifically targeting the youths to provide treatment and support for substance abuse;

Deeply concerned that the County lacks viable policies and legislation to regulate the sale and distribution of substances commonly abused by the youth, and to ensure the enforcement of existing laws related to substance abuse and mental health,

I, therefore urge this Assembly to RESOLVE:

1. THAT, the County government to expedite the establishment of well-equipped rehabilitation centers specifically targeting the youth to provide treatment and support for substance abuse, ensuring these centers offer comprehensive services including but not limited to counselling, vocational training and aftercare support;

2.THAT, the County government to encourage community-based initiatives and peer support groups to provide a network of support for the youth, promoting sports, arts and other extracurricular activities as positive outlets;

3. THAT, the County government, in collaboration with the National government Ministry of Education, shall implement programs in schools and communities to raise awareness about the dangers of substance abuse and the importance of mental health, utilizing media platforms to disseminate information and create a supporting dialogue around these issues;

4.THAT, the County government to increase the availability of mental health services within schools, community centers and hospitals and train healthcare providers, educators and community leaders to identify and address mental health issues early;

5. *THAT, the County government to advocate and formulate viable policies and review and enforce existing legislation to regulate the sale and distribution of substances commonly abused by the youth.*

May I ask Honourable Allen Katana to second the Motion. Thank you.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Yes, Honourable Allen Katana?

Hon. Katana: Thank you, Mr. Speaker. I stand to second the Motion. Thank you.

[Applause]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Honourable Members, I now propose a question that the Motion by Honourable Frankline Makanga on *Measures to Address Substance Abuse and Mental Health among the Youths in Mombasa County* be considered in this Honourable House?

[Question proposed and agreed to]

Yes, Honourable Makanga?

Hon. Makanga: Thank so much Mr. Speaker. Kwanza nianze na kuwakaribisha vijana wenza wa Mombasa jitambulisheni wale washajitambua ndio maana wako hapa na pia niseme karibuni sana kwa sababu naona ni vijana wenza almaarufu kile kizazi ambacho kimeweza kuleta mabadiliko katika Taifa la Kenya almaarufu Gen Z; ndio hawa na nafikiri hawajakuja kutusalimia lakini wamekuja katika mazungumzo kwa hivyo karibuni sana katika Bunge la Mombasa. Mimi ni Mwakilishi Wadi ya Chaani na karibuni, Mheshimiwa Spika nimesimama kuleta Hoja hii katika Bunge letu hili la tatu ambalo limejitwalia heshima kwa wananchi wake kwa sababu ya viongozi wakakamavu ambao wako katika Bunge hili. Mheshimiwa Spika kwa utangulizi ni kwamba Jumba hili likiwa Jumba la sheria na rekodi ni kwamba tulipoapishwa mwaka 2022, mwezi wa tisa baada ya mwezi mmoja kuliteuliwa jopo ambalo liliangazia maswala ya kiafya katika Kaunti yetu ya Mombasa. Mheshimiwa Spika, katika uteuzi wa jopo hilo kuna fedha ama rasilmali za kiserikali ikiwemo fedha na muda na *other infrastructure* zilitumika kuweza kutafuta ama kuweza kuangazia swala zima la afya katika mji wetu.

Mheshimiwa Spika katika mapendekezo mengi moja wapo hapa yaliyokuwepo ilikuwa kwamba kuweze kutengenezwa sehemu ama hospitali ambazo zitaangazia suala sugu la madawa ya kulevyia, ili kuweza kuwakamua ndugu zetu, vijana wetu na kwa wale ambao wana umri kiasi kama wewe Mheshimiwa Spika watoto wenu ili kuweza kuwatoa katika tatizo sugu la hawa vijana kuaharibika na mihadarati. Mheshimiwa Spika katika mapendekezo ambayo yako katika rekodi za Bunge hili; moja wapo ilikuwa kwamba hospitali zilizotajwa hapa ikiwemo Mrima ilioko Likoni na Marimani ilioko Mwakirunge Iikubalika kwamba hospitali hizo zitafanywa mahali kwa marekebisho kuwakwamua ndugu zetu, watoto wetu na jamaa zetu ambao wamekwama katika mihadarati Mheshimiwa Spika hilo likapitishwa na ripoti hiyo ikapelekwa kwa Gavana akaipokea na maamuzi pia ya kusimamamisha huduma za kawaida kwa hospitali kama vile Marimani ikafanyika na wananchi wakajulishwa na jambo hilo likazungumziwa, si kwa mikutano ya kisiri, si kwa mabaraza ikasemekana kila mahali hata kwa *social media* kwamba jambo hili litashughulikiwa.

Miaka miwili baadae Mheshimiwa Spika, jambo hili halijafanyika maamuzi hayo yaliyopitishwa katika Bunge hili hayajafanyiwa kazi na vijana wetu. Mheshimiwa Spika wanaendelea kuathirika na madawa haya ya kulevya. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika mimi ninaliomba Bunge hili kwamba tatizo hili la madawa ya kulevya tuliangalie kwa umaankini, kwa sababu endapo hatutaliangalia, endapo serikali haitawajibika na pesa za serikali zishatumika kuwalipa wale walikuwa wanaongoza jopo hilo Mheshimiwa Spika tutakuwa hatujaifanyia haki serikali, tutakuwa hatujafanyia haki wananchi wetu wa Mombasa. Mheshimiwa Spika kila siku tunapoishi leo hii ikiwa jumatano nina uhakika kuna kijana mahali ambaye anahangaika ya vile atajikwamua kutoka kwa madawa ya kulevya na Mheshimiwa Spika nikisema kwa kizungu *the longer we take the miserable our youth become*. Kwa hivyo sisi lazima katika Bunge hili kwa sababu tulipitisha na tukawaruhusu kutumia fedha na rasilimali za kiserikali lazima sisi kama Bunge tufanye wajibu wetu tuhakikishe ya kwamba yale yaliyopendekezwa na wananchi, yale yaliyopitishwa na Bunge hili, yale yaliyoko katika Bunge hili lenye nguvu sawa na *high court of the republic of Kenya* yaweze kufanyiwa kazi na hospitali hizo ziweze kufanyiwa kama ilivyopitishwa ili vijana wetu waache kuhangaika lakini waweze kuwa vijana ambao ni salama na kuweza kuishi maisha ya sawa ambao hawajaoa, waoe katika *gallery* kuna wasichana labda katika juhudi hizo wasichana pale watapata wakuwaoa vijana pale watapata wakuoa. Kwa hiyo mengi Mheshimiwa Spika naliomba Bunge hili tukufu aweze kuunga Hoja hii tuweze kupitisha tuweze kuwafanyia wananchi wa Mombasa kazi na mimi ninajua Mheshimiwa Spika wote nitaunga mkono hata shetani hata akitembea hapa baado yeye ataungan mkono. Ahsante sana Mheshimiwaa Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you Honourable Makanga. Yes, Honourable Allen Katana?

Hon. Katana: Mheshimiwa Spika kwanza nimshukuru Allah kwa kunijaalia kufika hapa siku ya leo. Pili, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii na pia nichukue nafasi hii kuwakaribisha wageni waliotembelea katika Jumba la watumwa wao hapa ili kuwaangalia wanavyofanya kazi zao. Mheshimiwa Spika rekodi za Bunge hili ni wazi zinaweza kusema kwamba mara nyingi nimekuwa nikipinga hoja zinazoletwa na Mheshimiwa Makanga. Lakini Hoja hii Mheshimiwa Spika nidhihirike wazi kuwa Mheshimiwa yoyote anayepanga kupinga hoja hii ni sawa na mchawi Mheshimiwa Spika...

[Applause]

Kwa sababu hoja hii Mheshimiwa Spika inaleta natija kwa kizazi chetu ambacho bila kufanya maombi haya yaliyoletwa na Mheshimiwa wa Chaani...

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): There is a point of Order! Yes, Honourable from Mikindani?

Hon. Madialo: Thank you Honourable Speaker. Honourable Speaker is Honourable from Shanzu in Order to allege that anybody with a contrary opinion is a witch yet he knows that in an Assembly...

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Honourable Member, are you up in a Standing Order or information?

Hon. Madialo: Is a point of order it does not matter which order but is he in order? To allege that that who has a contrary opinion is a witch yet he knows that in an Assembly or Parliament people have diverse views you are allowed to agree to the Motion or not to agree?

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Okay, Honourable Madialo, Honourable Allen Katana, please withdraw that statement?

Hon. Katana: Thank you. Honourable Speaker, you know it is only the old women who gets uncomfortable when you speak of dry bones...

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Just withdraw!

Hon. Katana: Honourable Speaker, you know when somebody asks for a point of order, he has to cite which point of order he is standing on. He did not cite...

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Withdraw!

Hon. Katana: Okay, I withdraw Honourable Speaker. I withdraw! Honourable Speaker, can I continue?

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Proceed.

Hon. Katana: Ahsante Mheshimiwa Spika. Unajua Mheshimiwa Spika...

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Yes, what is it Honourable Maryam Baimu?

Hon. Baimu: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Ningependelea ama kumuomba Mheshimiwa Katana aweze ku *retract statement* yake kutaja wanawake hapa!

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Honourable Katana, please proceed?

Hon. Katana: Unajua kiengereza kinatatiza sana! Huu ni msemo wenye uko na *phrase* zenye ziko kizungu na si mara nyingi watu wanasikia raha ukitaja mifupa mikavu, kwa kuwa inamridhisha Mheshimiwa Baimu sijui amesema ni *withdraw* ama amesemaje? lakini nakuridhisha pia...

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): So, you have withdrawn the statement?!

Hon. Katana: You have not asked me to, Honourable Speaker! So, allow me to proceed.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Then, withdraw!

Hon. Katana: No! Why should I withdraw, Honourable Speaker? You know, you are giving these people a say that is not there!

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Honourable...

[Interruption]

Hon. Katana: It is said, it is an English saying that it is only old women who get uncomfortable when you mention dry bones!

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Withdraw! Just withdraw Honourable Katana for you to proceed!

Hon. Katana: Mheshimiwa Spika...

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Just withdraw the statement!

Hon. Katana: Mheshimiwa Spika hii kazi unaifanya ngumu kwa sababu siko hapa kufundisha lugha watu...!

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): You will get a time...

[Interruption]

Hon. Katana: But for the sake... for the sake of continuing! Honourable Speaker, for the sake of continuing and to respect your position, I will listen and follow your directives *kwa watu ambao wanamatatizo ya kiingereza kidogo na withdraw ...*

[Applause]

Naweza kuendelea Mheshimiwa Spika?

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): What is it Honourable Leila?

[Interruption]

Hon. Katana: And kindly speak in English because I do not understand.

Hon. Nyache: Mheshimiwa Spika tunataka Mheshimiwa mwenza aweze kuheshimu kina mama na aheshimu wanawake kwa jumla...

[Applause]

Kwa sababu wao ndio wamemzaa na ndio waliomfanya mpaka akafika kwenye Bunge hili. Kwa hivyo tunaomba a *withdraw* hiyo *statement* kusema watu ambao hawasikii sijui hawafanyi nini, sijui wanawake hawajui kizungu twakuomba u *withdraw* hiyo *statement* yako ndio uendelee.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Okay Honourable Allen Katana, please withdraw!

Hon. Katana: Mheshimiwa Spika kwa sababu ajenda iliyo mbele yetu ni kubwa na ni ya maana kushinda huu ushindani unaoletwa hapa ku *withdraw withdraw! I withdraw!*

[Applause]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you.

Hon. Katana: Can I proceed?

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Proceed.

Hon. Katana: Mheshimiwa Spika, inanisikitisha sana wakati kumeletwa hoja ya maana, halafu kunakuja *drama* za *Tom and Jerry* na nangojea kwa hamu sana. Mheshimiwa Spika, atakayepinga swala la maana hili tutajua sijui alitumwa na na nani hapa?! Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa kuunga mkono hoja hii iliyoletwa na Mheshimiwa wa Chaani, daktari aliyeleta hoja hii ya kuhusiana na madawa na athari ya vitu ambavyo vijana wetu kwa wingi wanatumia na vile basi kuwafanya, wanakuwa hawana faida kwa jamii yetu. Mheshimiwa Spika, nataka kulieleza Bunge hili baada ya kutatizwa na maswala ambayo si ya uzito sana ni ya kwamba kabla maandamano ama huu mdahalo wa maandaano na mtafaruku wa nchi nzima kulikuwa kuna hoja inayouwiano na hii ya kwamba janga la *Mugoka* lilikuwa limetanda lilianza hapa kwetu Mombasa na likashika kasi Pwani nzima na likavaa kasi hiyo kenya nzima. Mheshimiwa Spika, kama unakumbuka na kwa kuwa vugu vugu hilo na fujo hizo zimetulia nataka nimpungeze sana Mheshimiwa Hossana kwa kuleta hii Hoja kwa wakati huu kwa sababu nilikuwa nina huzuni sana ya kwamba mchakato ulioanza hapa Mombasa wa kuleta mikakati ambayo italeta *control* ya hizi madawa na vitu ambavyo havistahili kutumika na watoto ilikuwa inaangamia. Mheshimiwa Spika, nikisema ya kwamba kuna hospitali kama ya Mrima na Marimani...

[The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Mwalimu Makarani) exited the Chair]

[The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir) in the Chair the Chair]

Mheshimiwa Spika ya kwamba hizi hospitali mbili Marimani na Mrima nashukuru sana kwa kukalia kiti hicho maana ulikuwa umepanga vitu ambavyo havina mana hapa...

[Applause]

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Order! Order! Order! Yes, Honourable *Bomoa* are you on a point of order? Are you on a point of order?

Hon. Omondi: Mr. Speaker, I'm up on a point of information, Mr. Speaker.

The Temporary Speaker (Hon. Abdiraman Abdikadir): Just relax, hold your horses!

Hon. Omondi: Mr. Speaker, I would like to inform the Member, who is using very harsh words, threatening words who has just spoken, that he is supposed to respect your Chair. Mr. Speaker, we know that you are a professional and we know that for you to sit on that seat, you have all it takes to be there so he should not question why you are there! Thank you so he should withdraw that statement with immediate effect.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Thank you Honourable *Bomoa* for coming up to my defense! Honourable Allen Katana you will not use your time to throw jabs at the Speaker, I will advise you to prosecute your agenda without further and unnecessary comments. Please proceed?

Hon. Katana: Ahsante Mheshimiwa Spika mimi nikiendelea Mheshimiwa Spika wengine pia wanafaa waniheshimu kwa sababu wamekuwa Wenyekiti baada ya mimi kiasi niwatulie ikiwa nimesimama Mheshimiwa Spika...

[Laughter]

Mheshimiwa Spika mimi sijui kwa nini Hoja ya maana hii inapewa mawimbi ambayo hayana maana. Mheshimiwa Spika hospitali ambazo zilikuwa zimewekwa na kutengwa kwa ajili ya kuwa *rehabilitation centers* na utanisamehe *for the lack of a better word* ya Kiswahili ya kusema *rehabilitation* lakini ni kwamba ni hospitali moja ya Marimani ambayo iko eneo Bunge la Kisauni, Mwakirunge na hospitali ambayo iko Mrima ambayo ni eneo Bunge la Likoni. Ninasikitika kutaja hapa kwamba na Mheshimiwa angekuwa hapa pia ningemwambia ni masikitiko makubwa kwa sababu tumekuwa kule Marimani na Mheshimiwa wa Mwakirunge akaomba hii *rehabilitation center* isiwekwe kule Mheshimiwa Spika. Mimi ni ombi langu japokuwa yale yalisemeka mtaani hayakusemeka katika Nyumba ya kupanga sheria na kupitisha bajeti Mheshimiwa Spika ni ombi langu Mwenyezi Mungu atakapotufaulisha na Waheshimiwa hapa ambao nawajua wana akili na hekma watakapopitisha hii ni kwamba iwe kila eneo Bunge la Mombasa yetu kuwe kuna *rehabilitation center* ya kuendelea kuwasaidia na nikiendelea...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Katana kindly wind up, you are taking too much time.

Hon. Katana: Mheshimiwa Spika ni watu wamenitatiza hapa si kupewa nafasi yangu...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Kindly wind up. Yes, are you up on the point of order?

Hon. Katana: Mheshimiwa Spika...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Are you up on the point of order Honourable Kai?

Hon. Kai: Yes, Mr. Speaker.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Will you be gracious enough to cite the Standing Order?

Hon. Kai: Naam, ningeomba Mheshimiwa Spika unajua hii ni Nyumba ambayo kila kitu kinachozungumza kinaweza kuwekwa kwenye rekodi na sijaona kama Mheshimiwa Mwinyi yuko hapa! Ninahisi sio sahihi kwa Mheshimiwa wa Shanzu kusimama mbele ya Bunge hili na kusema ya kwamba Mheshimiwa Mwinyi aliweza kusema ya kwamba hataki kitu cha muhimu kama hicho kiweze kujengwa katika Wadi yake ni kupotosha umma...

[Applause]

Na labda hapa kuna wananchi wa Mwakirunge wataondoka hapa wajue kwamba Mheshimiwa wa Mwakirunge alikataa huduma hiyo na maneno yake hatuwezi kuyathibitisha kwamba ni kweli Mheshimiwa Spika Mheshimiwa wa Mwakirunge alitamka hivyo...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Kai, are you sure that that is the statement Honourable Katana has made?

Hon. Kai: Mheshimiwa Spika ndio maana tuko na *Hansard* katika Jumba hili ni maneno ameyazungumza na naona yanaweza kuleta athari kubwa kwa wananchi na Mheshimiwa wa Mwakirunge.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Thank you. Honourable Katana, just confirm your position on that statement.

Hon. Katana: Mheshimiwa Spika kuna Waheshimiwa ambao wako tayari kupoteza muda utanipa nafasi yangu *because I have to transact this Business because this is the only business that brought me here, I understand and stop giving them chance to stand and giving Standing Orders without citing the Standing Orders because...*

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Katana...

[Interruption]

Hon. Katana: Standing Order Number 87 Mheshimiwa Spika...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Katana, Order! Order! Order! Honourable Katana...

[Interruption]

Hon. Katana: Standing Order Number 87...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Katana Order! Order! Honourable Katana I am advising you for the last time to watch your tone, to watch your language when you are addressing the Speaker and yes you are up on a point of order.

Hon. Omondi: Yes.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): I will not allow unnecessary interruptions going forward. Just cite the Standing Order please.

Hon. Omondi: Yes, I am not standing on an Order, am standing on a Point of information Mr. Speaker to this House. Mr. Speaker...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Are you seeking information or you want to inform us?

Hon. Omondi: I want to inform the House Mr. Speaker.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Ibrahim (Bomoa) just sit down, you will inform the House when your time comes, please!

[Interruption]

Hon. Omondi: On a point that was on aired Mr. Speaker.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Okay I will give you an opportunity to make your contribution to this Motion just take your seat.

Hon. Omondi: Thank you.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Katana, you have less than one minute to wind up.

Hon. Katana: Mheshimiwa Spika watu wa Shanzu hawakunituma nikiwa na akili punguani Standing Order 87 Mheshimiwa Spika inasema...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Katana we are past that...

[Interruption]

Hon. Katana: No Mr. Speaker am citing the Standing Orders you have given me one minute why are you limiting me.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Proceed?

Hon. Katana: Standing Order 87 inasema, *a Member shall be responsible for the accuracy of any facts which the Member alleges to be true and may be required to substantiate any such facts instantly!* Mimi Mheshimiwa Spika ninaloliongea nina uhakika nalo kwa sababu nilikuwa pale na ombi langu ikawa ni rai ya kwamba hizi *rehabilitation centers* Mheshimiwa Spika ziwekwe kwa kila eneo Bunge. Mheshimiwa Spika, mimi nikiwa shahidi hapa kuna shule ambazo ukitoka mita 100 bangi inauzwa hapo, *Muguka* unauzwa hapo. Mheshimiwa Spika sababu ya kusema mimi nitaunga mkono Hoja hii ni kwamba nimepeleka mimi mwenyewe na *if any Member want me to substantiate on whatever am saying* mimi mwenyewe nimepeleka vijana kumi na moja Port Reitz kwa sababu ya utumizi wa *Muguka*. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika tukisema mambo haya tunasema mambo haya ni ya kuungwa mkono kwa sababu tunaiona jamii yetu inaharibika lakini ikiwa kuna mtu leo hii anataka kusimama kwa kupinga Mheshimiwa Spika tuko tayari ipingwe lakini mwisho wa kwisha umma wa Mombasa utajua ni kiongozi nani anayetetea jamii yetu ya leo na jamii yetu ya kesho. Kwa hayo machache naomba kuunga mkono, naomba wale ambao wanapenda kupinga hata hoja za maana wasimame wapinge. Ahsante Mheshimiwa Spika.

[Applause]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Yes, Honourable Solomon Wainaina Ngugi?

Hon. Ngugi: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutufikisha hapa, pili niwakaribishe wageni wetu kwenye Jumba hili letu. Mheshimiwa Spika mimi nasimama kwa kuunga mkono Hoja ilioletwa hapa mbele...

[Applause]

Na itakuwa ni mara ya pili nikiregelea kuzungumza maneno haya Mheshimiwa Spika nilikuwa mmoja wapo wa waathiriwa wa haya madawa ya kulevya tunayazungumzia leo hapa...

[Applause]

Huu ni mwaka wa 20 tangu nijinasue na sikwenda *rehab* na kunao ndugu zangu ambao nimewaacha mpaka leo wanatumia hii mihadarati; wengine wameshakufa tumewazika. Hivi tunavyoongea kuna mmoja amekwama yuko Makadara nimtumiaji mihadarati hana kitambulisho anadaiwa laki mbili!

Watu huko mje wanashindwa watatoa wapi laki mbili waende wakamzike manake ilikuwa nimumiaji wa mihadarati, pia ilikuwa naomba hili Bunge kama wataweza kuwapa msaada hawa watu huyu aliyekwama watafute njia watu wao wapewe mwili waende wakamzike...

[Applause]

Inaniuma sana Mheshimiwa Spika jambo hili limezungumzwa na hii ni mara ya pili kuzungumzwa suala hili la madawa ya kulevyu hususan eneo letu tunalotoka sisi eneo la Nyali na Kisauni ndio tumeathiriwa haswa pakubwa imefikwa wakati hivi tunavyozungumzia si watu wazima mpaka watoto wa shule wanatumia hii mihadarati, si watumiaji pombe, si walaji muguka nitufanyeni tutakayoweza kufanya kwa uwezo wetu sisi tuliopewa tumtangulizeni Mungu mbele kuhakikisha tumewanasua watu kwa hili balaa. Kisa cha kufanya mimi niondoke kwenye mihadarati nilishikwa na TB nikapelekwa *rehab* nilichagua moja nipone TB ama nife na inatokea ubahatika watu wenye senti wakapelekwa *rehabilitation* lakini akitoka mazingira ni yale yale unakuta mtu ameregea pale pale kulingana tumeachia ni biashara ambayo inafanywa bila uoga na ikiwa tutachukua jukumu sisi kama Viongozi maana sisi ndio Serikali ya Mashinani tuanze kupigana sisi vita na haya mambo haitofanyika hii biashara...

[Applause]

Maana Mheshimiwa Wadi yako unayotoka kama kuna mtu yuafanya hii biashara wamjua vizuri sana huyu yuafanya na yuko *comfortable* yauza na wewe hata hulibebi ni sisi tuanze sisi maana usalama unaanza na sisi, sisi tulishike hili jambo na tuhakikishe kuwa isifanyike hiyo biashara si tu kuwapeleka *rehabilitation*, utampeleka *rehabilitation* akitoka uko pale wamsubiri yauziwa tena umebadilisha nini hatujabadilisha chochote. Ni hayo machache ahsante Mheshimiwa Spika.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honorable Members, even as we debate and ventilate on these issues, I would like us to restrict ourselves on the five prayers of this Motion let us not deviate from it, please. Yes, Honourable Hamisi Mbaya?

Hon. Hamisi Mbaya: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa hii niweze kuchangia kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu. Pili nimshukuru Mheshimiwa Mwenza ambaye ameleta Hoja hii tuweze kuijadili. Tatu niwakaribishe ndugu zetu ambao wameweza wametutembelea kuja kuona yale ambayo tunayafanya kama Wawakilishi wa Kata zetu. Nne nikimalizia nisiwe mwingi wa maneno ili nione kwamba nitaieleweka zaidi. Nimesimama kuunga mkono Hoja hii kwa asilimia 95. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Thank you. Yes, Honourable Juma Manuari, please make your contribution?

Hon. Juma Manuari: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Kwanza nimshukuru Manani kwa kutupa siku nyengine kwa afya, na pili niwakaribishe ndugu zetu, vijana wenzetu katika Jumba hili la utungaji sheria. Hapa ndipo yale mambo yenu ya Mombasa Kaunti yote yanapopikwa yakipikwa yanapelekwa yakipelekwa sasa kazi kwao wanaopelekwa, sasa sijui watayatenda ama watayaacha lakini sisi jukumu letu mlilotupa tutakuwa tumelifanya. Mimi nimesimama kwanza kumuunga kakangu kijana mwenzangu mkono kwa suala hilo kwa sababu waathirika wa madawa wako wengi ikiwa mimi mmoja wao pia tulipitia katika nyanja hizo.

Na leo ikiwa tumekaa katika Jumba hili saa zengine huwa tunazona zile athari za yale madawa maana hapa hapa naweza tibuliwa na hapa hapa nikarusha kinasauti bado zile athari ziko kichwani hazipotea! Mheshimiwa Spika katika maneno aliyoyatoa ndugu yetu, yale maombi aliyoyatoa ndugu yetu Bwana Mbega mimi namuongezea katika yale aliyoyasema. Tukishawawekea wale ndugu zetu hizi *rehab* kwa sababu saa hii tunayaona tuko nayo pale Frere Town na tuko na moja kule Kombani, lakini ni masikitiko mimi mwenyewe nilitembea kwenda kuangalia mtu akishamaliza kula *methadone* anazama nyuma hapo hapo nyuma bado anajibwenga na sio wote wanaokwenda kula *methadone* walikuwa wanakwenda kula *Methadone* kuna wengine pale wameenda kujiweka kama urafiki watengeneze kambi nyengine ya kutumia tena mihadarati.

Kwa hivyo Mheshimiwa Spika ndugu yetu ameelekeza sehemu mbili; Marimani na Mrima lakini ni pamoja na ndugu yangu Katana kuwa kila Wadi ama eneo Bunge kuwekwa hili suala la kuhakikisha tunawarekebisha watoto wetu ila tukirekebisha baada ya marekebisho wapi! Leo mimi nashukuru nilinusurika na leo niko Bungeni nilijipa shughuli wale watajirudia kwa kurudia, kurudia tutaleta makontena na meli za *methadone* katika hii Mombasa yetu lakini kusema ukweli kuwanasua itakuwa ngumu kwa sababu akitoka pale ana ajenda gani, rafiki yake anayemfuata ni nani, lakini bado watu wanarudi pale pale ndio unapata siku mbili tatu wametumia *methadone*, siku mbili tatu mdomo umeshambuka athari ya *methadone* iko ndani ya mwili wake na *still* anarudi anakwenda anatumia vile vitu vinavyotakiwa visitumike. Hivyo basi ni lazima sisi kama Wabunge na tukishirikiana na Gavana maana tunamsikia Gavana kila anapofika mahali, ‘mimi nitatengeneza’, lakini baada ya *methadone* ni nini, watoto wetu watafutiwe shughuli ya kufanya hizi ambazo twazileta sijui Mombasa ni yangu, sijui nini, sijui nini!

Mimi ningeomba hichi kinasauti hapa kipelekwe huko kama ni kuweka watu elfu tatu basi kuwekwa na watu elfu tatu wa juu wa kutumia yale madawa ili wakitoka pale wapewe shughuli na wao ya kufanya tukiwachokesha hawatakuwa na muda wa kuburura na tukiwa tumewaweka tusiwaweka katika nafasi za kazi za maeneo yao kwa sababu biashara iko pale pale atataka aende akapige vitu ndio apige kazi sasa tunawatoa kule na tunawapeleka sehemu zengine wiki inayofuata sehemu nyengine baada ya mwezi tukimaliza Mheshimiwa Spika itakuwa tumenasua vijana wetu wengi sana na mwisho Mheshimiwa Spika katika haya maswala ya mihadarati ata hili goka bado ni mihadarati mikubwa na naona sasa, kulikuja hoja ya Gen Z na wakafinika migoka imepotea. Hii ni swala goka na lirudishwe maana saa hii pale kwangu nasikitika nje ya shule kitu kinauzwa na tuliambiwa kumewekwa mikakati kila kona, hivi vitu viwe vimezuiwa visisumbuwe watoto wetu. Kwa hayo mengi na machache Mheshimiwa Spika naomba haya maswala yakizungumzwa hapa, yapelekwe na yafanyike na kama hafanyiki, tutatembea wenyewe ground. Ahsante.

[Applause]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Yes, Honourable Maryam Baimu, MCA Free Town please make your contribution.

Hon. Baimu: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipatia nafasi hii. Mimi kwanza ningeenda kumpongeza Mheshimiwa Hossana kwa kuleta hoja hii, kwa sababu ki mimi kwa kusema ukweli sehemu yangu ama Wadi yangu ni katika ile moja wao iliathirika sana na vijana kutumia hii mihadarati ambayo ni Wadi yangu ni Frere Town kama vile Mheshimiwa ameongelea hapo mbele.

Nikianza pointi yangu ya kwanza, nafikiria sote tunajua vijana wetu hawa ambao wanatumia hio *Mugoka* ama hayo madawa, tunaona sana wako na *depression* ama msongamano wa mawazo, wako na *anxiety* ama wasiwasi ndani ya nafsi zao na hata wengi wao tunaona mwisho wanaweza kujitia kitanzi ama kutoa uhai wao na kusema ule ukweli tunaona pia katika vijana wetu wanao tumia hii mihadarati, wengi tunaona wanaingilia sasa mambo ya uhalifu na pia tunaona wengi wanakataa shule na hata mwisho wanakuwa na shida za kiafya. Kwa hivyo kusema ule ukweli saa hii tukizunguka Mombasa yetu Mheshimiwa Spika tunaona wendawazimu wamekuwa wengi sana tena sana katika barabara zetu. Kusema ule ukweli vile Mheshimiwa Allen Katana ameongea, mimi mwenyewe kibinafsi nimeweza kupeleka watoto wanne wangu wa Frere Town Port Rietz Hospital katika hali ya wenda wazimu na tukidadi kule wale ambao wanahudumia hawa vijana wanasema asilimia kubwa ya watoto ambao wameathirika ya mambo ya wendawazimu, saa hata si mambo ya unga bali ni mambo ya *Mugoka*.

Kwa hivyo kusema ule ukweli iko haja yale mapendekezo tunapitisha katika hili Jumba, yaweze kutekelezwa na nikirudia nyuma kidogo, hii pendekezo la Mrima na Marimani kusema ule ukweli mimi kama Mwakilishi Wadi ya Frere Town nilikuwa nimefurahi sana kwa sababu pale kwangu kusema ukweli Waheshimiwa mkifika mtaweza kutokwa na machozi. Watoto wanatumia *Methodine* Kliniki wakitoka pale hakuna pahali wanaenda, wanakaa nyumba pale manake kuna *hall* ndio wanajijaza hapo utaona wasichana wadogo wamezaa wako na watoto wao hapo, wengine ni wagonjwa miguu inaoza, yaani ni hali ya kuhuzunisha. Sasa kwa sababu DCC aliwafurusha ama kuwa bumburisha pale hall, saa hii kuna nyumba wameenda hapo nyuma wanakaa siku nzima hakuna kitu wanafanya. Kwa hivyo mimi nilikuwa nimefurahi sana ilipokuwa tumepitisha kwa hili Jumba kwamba Mrima na Marimani, watoto watapelekwa pale na kusema ukweli, si tu kutumia dawa lakini pia pale ndani wafinyiwe *counselling*, pale ndani waweze kufanyiwa *vocational training* ili wakitoka pale mtoto atakuwa ana kitu ya kufanya aweze asirudi tena katika hali ya mihadarati...

[Applause]

Kwa hivyo maonit yangu ya mwisho ningemalizia ni kwamba kuhusu hii mambo ya shule na jamii, haya maongezi ama taarifa iwe inaweza kufanya hamasisho, watu waweze kueleza shule hatari za mihadarati. Nina imani tukishikana mikono hili jangwa la mihadarati Kaunti ya Mombasa tutaweza kulitupa kwa kaburi la sahai. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

[Applause]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Yes, Honourable Milka Areba please make your contribution.

Hon. Ngare: Thank you Mr. Speaker for the chance to also air my views. But before I do so I recognise that we do have guests in our gallery and may I take this opportunity to welcome them and tell them to feel at home in this Honourable House. I am up to support the Motion...

[Applause]

Brought by Honourable Makanga of Chaani Ward. It is a Motion that has a lot of weight and I have seen before this Motion I have seen similar but I have looked at the prayers of today very critically and I will zero in on prayer number 2 and 3.

Waswahili wanasema, “samaki mkunje angali mbichi”! The issue of use of drugs starts at a very early age and we have young children; I have heard Speaker after Speaker and they are narrating issues of what they have undergone and what they have experienced in their Wards and even themselves as Honourable Members here so when young children have started abusing drugs, they get in to mental health issues that cause a lot of miseries in our homes and in our community at large. Prayer number three talks of schools. Honourable Manuari has talked about these things recurring all the time us talking all the time. We need to have the school going children even at a very early age being sensitized through the programs of the County government, so that they can get to understand the dangers of abusing drugs. The late Honourable Michuki caused a big impact in the Transport industry why? Because people were taken through why they must tie their belts while they are in the vehicle. They were told that when you tie your belt the impact of an accident is not going to be as bad as a person who has not tied their belt and people got to understand and there was a big reduction in our country on road accidents.

He took that initiative so we must as a County government take a initiative of doing programs in schools while the children are still young, we educate them, do serious programs, we educate them so that they get to understand we might reduce and for sure we will reduce the use of drugs within our County government, I really support prayer number two and three. Start from the schools and the children will get to understand and even if they come across the drugs, they will evade them because they have already been told the side effects. So, I support this motion in totality, I support the sentiment that has been aired by my fellow Honourable Members, I saw Honourable Katana really very aggressive on the same, I support the sentiments and all other all Honourable Members who have talked. Let us support the motion and follow it up later through the executive wing, follow this to the letter so that we get to curb the usage of drugs in our County. Thank you, Mr. Speaker.

[Applause]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Yes, Honourable Silvester Kai please make your contribution.

Hon. Kai: Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa niweze kuongea nimetamani nionge kitambo lakini kwa sababu Kenya ni nchi ya kuheshimu dada zetu, nimeona ukiwapatia kipao mbele lakini nilivyoona mwenye amesimama ni Mwenza wa chama changu cha UDA nikajua nafasi lazima nitapewa...

[Laughter]

Basi nichukue fursa hii kwanza kuweza kuwaalika wageni wetu wa siku ya leo, ili mkaweze kupata fursa ya kuona Jumba hili lenye nidhamu, linaendesha shughuli ambazo mliweza kutukabidhi. Kwanza kabisa ningependa kumshukuru ndugu yangu Mheshimiwa wa Chaani Makanga kwa kuweza kuleta hoja hii ya maana kubwa sana...

[Applause]

Japo kuna wachache ambao wanatakla kuifanya kama ni yao lakini ni lazima nisisitize ya kwamba imeletwa na Mheshimiwa Makanga...

[Applause]

Basi mimi nichukue fursa hii Mheshimiwa Spika kusema ya kwamba ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia tisaini na tisa kwa sababu ni janga ambalo limeweza kuathiri Mombasa nzima limeweza kuathiri kila Mheshimiwa katika maeneo ambayo anaweza kutoka. Hivyo siwezi nikaona ya kwamba kuna kunaweza kukakuwa na punguani katika Jumba hili akaweza kupinga hoja muhimu kama hii...

[Applause]

Hii nimeweza kuona Waheshimiwa wenzangu watangulizi wamesema mambo mingi ambayo madhara tunaweza kuyapata mbali mbali, lakini pia tunaamini kiafrika ya kwamba kuna haja unapokuwa na kuweza kufikia umri fulani, unatarajiwa kuanzisha familia lakini kwa sababu ya majanga ya mihadarati, unakuta kwamba watu wengi wameweza kukosa kuchukua jukumu lile la kimsingi la kuweza kuanzisha familia lakini vile vile pia, Mheshimiwa Spika hata wale ambao wameanzisha familia wameweza kukosa kuzikimu hivyo imeweza kuchangia kua na vijana wingi ambao tunasema ni *street boys* and kwa sababu, ya kwamba wazazi wamekosa kuchukua majukumu ya kimsingi kwa sababu ya kwamba wameweza kujiingiza katika jinamizi hili. Hivyo basi niungane na wenzangu kusema ya kwamba tuweze kupitisha hoja hii ama Mswada huu, lakini pia tukaweze kuomba wale ambao ni watendaji wakaweze kuhahakisha ya kwamba, yale yote ambao tayari washaweka kwenye mikakati kama vile mrima marimani, yakaweze kutekelezwa lakini pia tutaweza kukaa na tuangalie ni yapi mengine ambayo tunaweza kuyachukulia na uzito, ili swala hili likaweze kutusaidia kutoa jamii zetu katika mitihani hii. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

[Applause]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Thank you. Yes, Honourable Samuel Mwaura MCA Kongowea Chairman of Implementation Committee.

Hon. Mwaura: Thank you Mr. Speaker for giving me this opportunity just to hear my voice towards these very good Motions, but even before I do so let me join my colleagues in welcoming the Juhudi Initiative Members into this Chamber.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): It is the, just get their name right please.

Hon. Mwaura: Thank you as I welcome them let me...

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Mombasa Jitambue Initiative...

Hon. Mwaura: Let me introduce myself, I am Samuel Mwaura from Kongowea Ward. Mr. Speaker, this Motion comes a time that we have visitors who are youths in this Assembly. Whether it is a coincidence or otherwise Mr. Speaker, it must be appreciated and they have also seen that this House really is concerned about our youth. Mr. Speaker, I do want to say that this Motion really touches on every other Member in this Assembly; right in Kongowea Market we have drugs being traded there and we really need those kids to be saved from the menace.

I do support the expeditation of the establishment of these centres so that we may save our youths from the menace. So, Mr. Speaker, I do support. Thank you.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Welcome to the chambers, Honorable Prischillah. Yes, Honourable Ibrahim *Bomoa*. Please be brief.

Hon. Omondi: Thank you, Mr. Speaker, for the humble opportunity given me. Mr. Speaker, just to acknowledge the members from Jitambulish Kenya *karibuni sana*. Having gone through this particular Motion, Mr. Speaker, I want to stand with the fellow Members of this Honourable House to support this particular Motion, and also, to support or to congratulate a Member of Chaani, Honourable *Hossana*. Mr. Speaker you know, we know very well that the electorate gave us the power and the will to come in this Honourable House to represent them on the issues that are affecting them on the ground. On the issue that we are discussing today in this particular Motion, I can say is an elephant in the House Mr. Speaker! We all know that youths are the most productive and active regime that in society and that we are looking upon to redeem us from very many things in terms of production and other things. Mr. Speaker if we miss it, if we are not careful, we are going to miss the whole point and therefore we are going to lose the whole regime in future. So, we must be very careful at this particular point Mr. Speaker and I want also to say that we shall be judged harshly if we are not going to actually look into this particular issue critically. We shall be judged, during the time of judgment, we shall be judged harshly and remember you will also be in that line of judgment!

Mr. Speaker, I want, before I conclude, I just want to thank or to acknowledge some of the departments and private sectors that are doing good work on this matter. Mr. Speaker, I want to recognize the SHOFCO who are doing so much well on this part and they are promoting, they are helping us on mental health. They have set up several centres in different parts of the County Mr. Speaker where these centres are there to help the youths on the issue of mental health. Mr. Speaker, I also want to applaud the County government of Mombasa through the Department of Education, where I chair that the Governor has come up with this initiative of *Mombasa Yangu*, whereby we all know that idleness is the workshop, is actually makes the youths to become idle and eventually participate in these crimes and other unworthy activities. So, the Governor, having come up with this *Mombasa Yangu* is occupying the youths, Mr. Speaker. Just to say, Mr. Speaker, that this House should come out with policies and legislation which are friendly to the youths that are going to support them. Mr. Speaker, very many people have talked about awareness, educating the youths, creating avenues where the youths can go and do some activities like these employment opportunities and so on and so forth and by doing that obviously I know that this matter will come to rest and one day, in Mombasa people will not call this County a County of drugs. Thank you, Mr. Speaker, I support.

[Applause]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Ibrahim, before you finish are you supporting the Motion in totality?

Hon. Omondi: Yes, of course, Mr. Speaker. Following my sentiments Mr. Speaker of course I'm supporting the Motion. Thank you.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Okay, I wanted to get that clear. Yes, Honourable Jactone Madialo.

Hon. Madialo: Thank you Mr. Speaker I do support.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Thank you. Yes, Honourable Leila.

Hon. Nyache: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kuniona japo kuwa nimefanya zoezi nimesimama nikikaa angalau unione lakini nashukuru saa hii umeniona. Nimesimama kwanza kuunga mkono hoja hii na pia kuwakaribisha Mombasa *Tujitambue group* karibuni sana. Karibuni katika Bunge la Mombasa mujiskie muko nyumbani na muone vile tunawakilisha wananchi ama tunavyowakilisha nyinyi pia huko mashinani. Karibuni! Mheshimiwa Spika nataka nimshukuru Mheshimiwa mwenza Bwana *Hossana* ambaye ni jirani yangu kule Chaani kwa kuweza kuleta hoja nzuri kama hii ambaye itaweza kusaidia watoto wetu. Nataka niseme hivi hoja hii Bunge lililopita pia iliweza kuja hapa kuletwa na Mheshimiwa Hamida na haikuweza kutekelezwa; kwa hivyo tunaomba hii ya sasa imeletwa na Mheshimiwa Makanga iweze kutekelezwa kwa sababu ni masikitiko sana kuona watoto wetu wanaangamia kupitia madawa ya kulevya. Kupitia hiyo *Migukaa* ni swala la kusikitisha sana na sisi viongozi tuko, wazazi wako, walimu tuko; ni masikitiko makubwa sana na pia ningependa tujiulize haya madawa kwanza yanatoka wapi na yanakuja na kina nani. Hatukuanza hivi vita leo, zinapita na wapi hivi vita tumevianza kitambo sana kunasua watoto wetu kutoka madawa ya kulevya lakini tunakuta yanaendelea kisiri hatujui ni nani.

Kwa hivyo sisi tunaomba kama viongozi vile tunavyoleta Mswada hapa na kuweza kutunga sheria jamani ziweze kutekelezwa na hao wanaoleta hizi dawa pia jamani watusikie sisi hapa katika serikali ya Kaunti ya Mombasa tunapigana na hizo madawa kwa sababu watoto wetu wanaharibika. Mimi nataka kusema huu msongo wa mawazo pia umeathiri wazazi, yule mtoto ameathirika kwa ajili ya madawa, mzazi amethirika kwa sababu yule mtoto amemzaa aweze kumsaidia ama amemsomesha aweze kujimudu maisha yake lakini unakuta mtoto hawezi kujimudu maisha yake. Ni mtoto wa kiume amekuwa ni borohoa hata hajielewi na wewe unajijua mzazi umezaa mtoto wa kiume; mimi nataka kutoa mfano ulioko hai kule kwangu. Mimi natoka Wadi ya Kipevu, kwangu mimi kuna kijana yeye ambaye sasa mimi nilielezewa kwamba yeye ni bibi ya ile kundi pale, ni sawa kweli? Na ni mtoto mzuri amesoma vizuri, mtoto ameelimishwa vizuri kwao kuna kila kitu lakini mtoto ametumia madawa ya kulevya mpaka ameharibika hajiwezi wala sio mume tena! Yule mama pia amekaa kama kuchanganyikiwa na babake pia yaani hawana uso kwa sababu ya yale mtoto wao anafanya pale mtaani na ni jambo la kusikitisha sana. Kwa hivyo mimi napongeza sana na naomba serikali ya Kaunti iweze kupanga kama tutaweza kuja na jopo ambalo litaweza kuzunguka katika hizi shule zetu zikiweza kuhamasisha watoto wetu katika mashule na ziweze kuzunguka hata kama ni hizi baraza za Chifu, waweze kuhamasisha palepale na pia kuwe na *rehabilitation centres* kama itawezekana iwe Mrima na Marimani iweze kuwekwa madawa vizuri na kuwekwe usalama. Mimi nimesikia kwamba wanakunywa madawa na tena wanazunguka huko nyuma na kujibwenga, sasa kuwekwe pia usalama wale wanaokunywa madawa watulie palepale yule anayekuja na yale madawa pale nyuma kwa ile *rehabilitation centre* aweze kushikwa kwa sababu tutakuwa tunafanya mchezo wa *merry go round*. Tunaenda mbele tukirudi nyuma watoto wetu wapewe dawa tena wazunguke nyuma wapewe tena madawa hiyo itakuwa tunafanya *zero work*. Kwa hivyo tunaomba pia ikuwe na usalama katika hizo *rehabilitation centre* na pia vile nimesikia ni vijana kuna wazee wameathirika na haya madawa ya kulevya pia...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Your time is up Honourable Leila! Thank you for your contribution.

Hon. Nyache: Sawa nimesimama kuunga hoja hii mia fil mia! Ahsante Mheshimiwa Spika. Ahsanteni nyote na ningeomba Waheshimiwa wenzangu wasimame waunge mkono.

[Applause]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Members, I think...Okay Honourable Fatma Mote. Please be brief.

Hon. Fatma Swaleh: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kuweza kunipa fursa hii. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu, muumba mbingu na ardhi pasi na kizuizi. Pili, Mheshimiwa Spika naomba kwa rukhsa yako namshukuru Raisi wetu wa Jamhuri ya Kenya kwa kuweza kutuchagulia Waziri ambae sio mwengine ni Ali Hassan Joho vilevile Mheshimiwa Spika najua bado chama kitakuwa imara hapa kwetu Mombasa...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Fatma, I will not allow you to get away with that! We are dealing with a Motion by Honourable Frankline please desist from bringing in unnecessary topics into this Motion. I hope you are guided.

Hon. Fatma Swaleh: Mheshimiwa Spika kabla sijaongea nimekwambia kwa rukhsa yako na mimi natoka Mombasa na lazima nijifarague na lazima nifurahie na kama nina makosa unambie.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Una makosa Mheshimiwa Fatma!

Hon. Fatma Swaleh: Aaah haya wacha niendeleo na mada Mheshimiwa Spika. Lakini umenitoa upepo Mheshimiwa Spika...

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Proceed please.

Hon. Fatma Swaleh: Mimi pia nimesimama kupongeza; naomba munielwe kwa makini, nimesimama kupongeza! Kuna tofauti ya kuunga na kupongeza; hivyo ni vitu viwili tofauti kwa sababu wale ambao walikuwa hapa muhula uliopita waliweza kuleta Mswada kama huu ndani ya hili Bunge tukufu la heshima wale walikuwa hapa mashahidi wangu kama vile Mheshimiwa alivyozungumza Mheshimiwa Leila kwamba huu Mswada ulikua hapa. Cha kusikitisha na kutamausha ni utekelezaji hakuna na kando na hivyo Mheshimiwa Spika kuna watu ambao huwa wanapata pesa kwa mashirika lakini sijaona mashirika huwa naona machache lakini wengi wanapokea pesa kutoka kwa wafadhili. Mheshimiwa Spika, naomba munielwe kwa makini Waheshimiwa wenza tusije hapa tunaregelea Mswada tunaregelea hoja lakini hakuna utekelezaji na pia tujue sababu ni nini! Maana yake Mheshimiwa Spika jambo la kusikitisha siku hizi hata sisi wazazi tunakula Migokaa ndani ya nyumba zetu. Tunaanza na wapi Mheshimiwa Spika, kabla hatujapitisha sheria, wajua sio kwamba namkosoa Mheshimiwa mwenzangu lakini tuanze ndoa nyingi siku hizi zinakatika.

Hii ni kwa sababu ya nini, *jaba!* Na *jaba* ni mihadarati....

[Interruption]

Mheshimiwa Spika naomba unikinge na Mheshimiwa Makanga namuona ananung'unika!

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdirahman): Yes, proceed please.

Hon. Fatma Swaleh: Lazima tujue chanzo ni nini?! Sio kila siku tunakuja na Miswada Miswada hautekelezwi Mheshimiwa Spika ndani ya majumba watoto wanakula *majaba*, kina mama ndoa zinavunjika, sisi wenyewe kina mama siku hizi tunakaa tukila majaba na watoto wetu ndani ya majumba. Mimi ningefurahi sana kuona mashirika wanafanya mikutano mashinani wakihamasisha watu maanake mashirika hupata pesa Mheshimiwa Spika, lakini ile ya kwanza tuliunga na hii tukiunga tutakuwa sisi twaunga, twaunga lakini hakuna utekelezaji na siku hizi madawa ya kulevya sio lazima iwe *Mugokaa* hata simu siku hizi sisi wengine tumekuwa mateja wa simu Mheshimiwa Spika. Tumekuwa mateja wa simu hatuna mda na watoto wetu, hatuangukii watoto wanatumia nini, wanatumia vileo gani Mheshimiwa Spika. Kwanza hili Bunge ikiwezekana watumie kabambe Mheshimiwa Spika maana yake ukiangalia ukikaa hapa wengine ndio hawa, sitaji mtu utamuona mtu anaangalia chini hizi ziweze kuzuiwa pale ama sivyo hapa Waheshimiwa watumie kabambe.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Fatma, you are out of order and out of topic! Come back to the topic.

Hon. Fatma Swaleh: Mheshimiwa Spika, nafikiri tunazungumzia kuhusu mihadarati, mihadarati iko aina nyingi...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Yes, Honourable Priscillah, are you up on a point of order? Take your seat Honourable Fatma.

Hon. Mumba: Mheshimiwa Spika nataka kusimama na kujuza Nyumba hii, sio kujuza anaezungumza, nasimama kwa ajili ya kujuza Nyumba hii. Sasa sisi tunazungumzia mihadarati ya nje, nashangaa tunaanza kutandikwa hapa ndani na ni Mheshimiwa mwenzetu anae tutandika! Yeye mwenyewe ana simu ya tachi mkononi, yeye mwenyewe ana vitu vya kila aina hata ukimuangalia pengine amekula huo mugokaa ndio akaingia hapa...

[Laughter]

Kwa hivyo asituambie sisi tumetatizika hapa ndani ya hili Jumba. Mheshimiwa Spika tunazungumzia wananchi wetu ambao wako nje, sisi ni viongozi na tunajielewa tukiwa hapa lakini kama ni teja wa kwanza, ni Mheshimiwa Swaleh Mote Fatma ndio alafu aendelee kueleza wengine! Kwa heshima hili ni Jumba la heshima na tunataka pia yeye atuheshimu kama Waheshimiwa wenzake, kama yeye ni teja, sisi sio mateja lakini yeye ni teja.

[Applause]

Hon. Fatma Swaleh: Mheshimiwa Spika.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Take your seat please!

Hon. Fatma Swaleh: Mheshimiwa Spika ni hujuma unanifanyia.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Prischilla, you have made some grave allegations! You have alleged that she might have consumed *Mugoka* before she came to these chambers; you know, the procedure here it is either you substantiate that you saw her or you have seen her buy it, consume it or you just withdraw it for the purpose of Hansard please.

Hon. Mumba: Mheshimiwa Spika, nakupa Kiti chako heshima na nakuheshimu lakini tukija tukiambiwa sisi hapa tuko mateja wa simu, angalia uzito wa jambo lile kama Mheshimiwa ni mtu angekuwa yuko haswa timamu anaweza kusema Waheshimiwa wenzake ni mateja hapa ndani ya Nyumba?! Mheshimiwa Spika, mimi namuheshimu ndio maana unasikia ninasema kama yeye amesema sisi huku ni mateja wa simu basi yeye ni teja wa *Mugokaa*, ndio akaingia hapa akazungumza maneno yale. Mheshimiwa Spika naheshimu Nyumba hii na naheshimu Kiti chakolakini ikiwa mimi nimeitwa teja wasimu, basi yeye ameanza na mugoka ndio akarudi akawa teja wa simu, simple Mheshimiwa Spika.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Just withdraw it! Will you be kind enough to withdraw that statement?! I will ask her to withdraw it as well.

Hon. Mumba: Mimi na *withdraw* kwa sababu Mheshimiwa Spika sina makubwa lakini asituite mateja wa simu hapa ndani ya Nyumba. Ahsante Mheshimiwa Spika.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Fatima. Please stick to the Motion and do not respond to Honourable Priscilla.

Hon. Fatma Swaleh: Mheshimiwa Spika, kwanza ukisema nisijibu kwa Mheshimiwa Sheilla itakuwa kwanza ni hujuma na ni matusi makubwa kwa Wapambe wetu wa Bunge nafikiri kabla hujaingia hapa, Wapambe wako pale huwa wanatukagua vizuri ili tuingie. Vile vile Mheshimiwa Spika mimi ni mke wa mtu, Mheshimiwa Sheilla atasemaje mimi natumia *Mugoka*, nikipewa talaka kama leo?! Kwa kuweza kutumia mihadarati Mheshimiwa Spika, kwa tuhuma Mheshimiwa ambayo Sheilla anakuja nayo Mheshimiwa Spika. Sawa Mheshimiwa Spika ni hujuma nimepata leo.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Mheshimiwa Leila are you also touched by those sentiments?

Hon. Nyache: Mheshimiwa Spika, mimi naheshimu Kiti chako na ningekuomba tuendelee na hii hoja, hii hoja ni nzuri Mheshimiwa Spika na itaweza kuleta natija kule nje, kwa hivyo tuwache stori nyingi.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Let us..., *tuwache stori za jaba*. Let us continue with the topic that is at hand!

Hon. Fatma Swaleh: Mheshimiwa wajuwa hakuna stori za jaba ikiwa umepewa mic hujuwu kujieleza, wacha sisi ambao twajuwa kujieleza tujieleze na tuzungumze hili swala kwa kina Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika kama nilivyozungumza hapo awali kuna mihadarati aina nyingi, na huu mswada Mheshimiwa Spika ushaletwa hapa. Mimi nimesimama hapa kuunga mkono huu mswada lakini Mheshimiwa Spika, napeleka kidole cha lawama kwa Mheshimiwa Mwaura kwa sababu yeye ndio Mheshimiwa wakufanya implementation si tuingie ndani ya hili Bunge tuilete miswada, miswada yenyewe haitekelezwi. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Thank you. Honourable Members, I think we have fully exhausted this Motion unless, someone really has the urge to contribute. Yes, Honourable Hawa last person to contribute.

Hon. Hawa Abdulrahman: Thank you, Mr. Speaker for giving me this opportunity to contribute to the Motion of measures to address substance and mental health among the youth in Mombasa County. Mr. Speaker, before I contribute, I would like to take this opportunity to recognize and welcome my fellow youth from the initiative. The Motion is precise and also timely because it concerns the emerging issues that I believe the initiative addresses every day. I also believe that you will carry some knowledge with you when you address your community. Mr. Speaker, I support the resolutions and prayers to this House subjected to this House by Honourable Makanga they are well presented and also if implemented, I repeat, if implemented because when it comes to implementation, that is where we draw the line if implemented, we will make a bigger step to controlling this issue of substance abuse and mental health among the youth. I would like to congratulate Honourable Makanga for specifically insisting on this age gap of the youth because it is at this stage where most people engage in substance abuse and also, they get affected mentally, they lose opportunities. Most of the opportunities pass them by because of substance abuse and also the issues of mental health so, this motion is timely and precise and without taking more time, I would like to support the motion. Thank you.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Thank you, Honourable Hawa. Yes, Honourable Frankline Makanga, the mover of the Motion. Please reply to the Motion.

Hon. Makanga: Thank you so much Mr. Speaker and allow me to thank the Honourable Members who have for the last two hours debated on this Motion. *Mheshimiwa Spika niwashukuru kwanza kwa sababu ya changizo zao na labda kwa kulifahamisha ama kuwaeleza wenzetu kwamba tofauti ya hoja hii na iliyoletwa hapo nyuma ni kwamba haya tunayo yazungumzia katika hoja hii ni mapendekezo ambayo yalikuwa kwa taskforce report na ningeomba Mheshimiwa Spika endapo Kiti chako utaweza kupeana maagizo ili Mheshimiwa kama Mheshimiwa Fatma Mote aweze kuyasikia haya ninayoyasema ya kwamba haya ambayo tunayazungumzia si hoja kwa sababu ni maswala yanayochimbuka lakini ni maswala ambayo rasimali za serikali zilitumika, mapendekezo yakaletwa, kuna watu wakalipwa mshahara walipoteuliwa na Gavana kufanya zoezi hili na Bunge hili likapitisha. Kwa hivyo ni wajibu wetu sisi sote bila kunyooshea mtu yeyote kidole cha lawama kufanya kazi yetu ya kuhakikisha yanayopitishwa katika Bunge hili, yanafanyiwa kazi. Mheshimiwa Spika, vile vile katika maombi yangu ambayo nimeomba labda kuendelea kuyapigia upatu tukianza na nambari moja tunaposema hawa watu wafanyiwe comprehensive services endapo mtu ana uwezo wa kusoma hisia ambazo Mheshimiwa Ngugi ameelezea akiwa mmoja wa wale ambao aliathirika na madawa ya kulevya, Mheshimiwa Spika utapata ya kwamba ni jambo ambalo linahuzunisha sana.*

Mheshimiwa Spika hoja ya kwanza ambalo ni ombi ambalo tungeomba tupitishe nikiwa najibu ni kwamba naongezea ili wanapopiga kura wajue wanapiga vipi Mheshimiwa Spika...

[Interruption]

Nakuomba dakika moja na nusu nitakuwa nisha maliza...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Frankline, this matter has been debated extensively and I think all Members have agreed to this Motion so please just be brief.

Hon. Makanga: Thank you Mr. Speaker. Therefore, I request the Honourable Members who are here *pamoja na changizo zao ambazo wametoa, mambo haya ambayo tumeomba kama maombi tuyapitishe na tufatilie* Wizara ya Michezo wametajwa hapa wahusike kikamilifu *and all other relevant departments so that we can save our generation not only for us but for the many years to come, that we shall make Mombasa great again. Thank you so much and thank you Honourable Members.*

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Thank you. Honourable Members, I now put the question that Motion by Honourable Frankline Makanga on measures to address substance abuse and mental health among the youths in Mombasa County be considered by this Honourable House in the same terms as moved.

[Question put and agreed to]

[Applause]

Honourable Members, the Motion by Honourable Frankline Makanga on measures to address substance abuse and mental health among the youths in Mombasa County is adopted by the House. Yes, Clerk?

ADJOURNMENT

Honourable Members, thank you for your time. This House stands adjourned until Wednesday, 31st July, 2024 at 2:30p.m. Thank you.

The House rose at 11:43a.m.